

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI

28 JUNI, 2016



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA MBILI – 28 JUNI, 2016

I. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

443. MHESHIMIWA STANSLAUS HAROON NYONGO (MASWA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Hospitali ya Wilaya ya Maswa ina uwezo mkubwa wa kuhudumia Wananchi wa Mkoa wa Simiyu:-

Je, ni lini Hospitali hiyo itapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa.

444. MHESHIMIWA DESDERIUS JOHN MIPATA (NKASI KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namanyere imetimiza vigezo vyote vya kuwa Halmashauri ya Mji:-

Je, ni lini Serikali itaipa hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji Mamlaka hiyo ya Mji mdogo wa Namanyere.

**445. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE
(MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Moja kati ya vikwazo vikubwa vya utekelezaji wa Ilani ya CCM ni kutotolewa kwa fedha kwa ukamilifu na kwa wakati:-

- (a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilikasimiwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kwa mwaka wa Fedha 2015/2016;
- (b) Je, Serikali imetoa kiasi gani cha fedha za Miradi ya Maendeleo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Msalala hadi kufikia Desemba, 2015;
- (c) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha fedha za maendeleo zinapatikana kwa wakati na kupelekwa kwenye Miradi husika.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

**446. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA
(MAKAMBAKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Miradi ya maji ya Manga pamoja na Kijiji cha Mutulingara inasuasua tu mpaka sasa:-

Je, ni lini Miradi hiyo itapatiwa fedha ili iweze kukamilika.

**447. MHESHIMIWA CATHERINE VALENTINE MAGIGE
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, ni lini mradi mkubwa wa maji Wilayani Longido utaanza rasmi ambao utakuwa ni mkombozi kwa Wananchi wote wa Wilaya ya Longido.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

**448. MHESHIMIWA HASANI ELIAS MASALA
(NACHINGWEA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Nachingwea ni miongoni mwa Wilaya chache zilizo na historia ndefu katika kusaidia nchi nyingi za Afrika kupata uhuru; kwani wapiganaji wengi wa nchi hizo walihifadhiwa kwenye Kambi ya Ukombozi ya Farm 17 iliyopo Nachingwea:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya Kambi ya Farm 17 hata kama yamegeuzwa kuwa Sekondari ili kuwa maeneo ya kihistoria na kuweza kuwavutia Watalii;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzishawishi nchi zilizonufaika na Kambi ya Farm 17 kama Msumbiji na Zimbabwe ili ziangalie kwa karibu

Kambi hiyo kwa lengo la kuhifadhi kumbukumbu muhimu zilizopo.

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

449. MHESHIMIWA JORAM ISMAEL HONGOLI (LUPEMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Serikali ya Awamu ya Nne ilianzisha utaratibu wa mbolea za ruzuku ili kuwasaidia wakulima wasio na uwezo wa kununua pembejeo waweze kuzipata na kuboresha kilimo:-

- (a) Je, Serikali haioni kama inapoteza fedha nyingi kusambaza pembejeo hizo kupitia mawakala ambao mahali pengine hupeleka mbolea kidogo au wanawasainisha wakulima vocha bila kuwapa mbolea kwa kuwapatia Tshs. 5,000/= - 10,000/= na baadaye kurejesha mbolea mahali pengine;
- (b) Je, kwa nini Serikali isisambaze mbolea hizo kupitia Kamati za Ulinzi na Usalama kuliko hao Mawakala ambao sio waaminifu.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

450. MHESHIMIWA SUSAN CHOGISASI MGONOKULIMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Mfumo wa mashine za EFDs hauchanganui kwa uwazi fedha ipi ni mapato ya kodi na ipi ni faini au ni gharama za uendeshaji:-

Je, ni lini kutakuwepo ushirikishwaji kati ya waandaaji wa mfumo wa TRA na viongozi wa wafanyabiashara ili kodi inayotozwa iwe halali na isiwe inayoua mitaji ya wafanyabiashara.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

451. MHESHIMIWA YUSSUF SALIM HUSSEIN (CHAMBANI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Suala la raia kupigwa na kuharibiwa mali zao kwa upande wa Zanzibar limekuwa likiongezeka siku hadi siku:-

Je, Serikali inatambua tatizo hili, na kama inalitambua inachukua hatua gani.

II. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na
Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2016 [*The Public Procurement (Amendment) Bill, 2016*].

**DODOMA
28 JUNI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**